**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa )**

**WITO KWA WASANII KUSHIRIKI KATIKA**
**TAMASHA LA 44 LA KIMATAIFA LA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO**
**KUANZIA TAREHE 28 HADI 31 OKTOBA 2026**

## UTANGULIZI:

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (***Zamani ikijulikana kama Chuo Cha Sanaa Bagamoyo***) inawakaribisha wasanii binafsi na vikundi kutoka sehemu mbalimbali duniani kuomba kushiriki katika Tamasha ambalo litakalofanyika katika viwanja na kumbi za Taasisi **(TaSUBa - Bagamoyo)** kuanzia tarehe **28 hadi 31 Oktoba 2026**, katika mji wa kihistoria wa Bagamoyo, Tanzania.

## KUHUSU TAMASHA:

Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo ni tukio ambalo ni la kipekee na lenye kuvutia sana. Kwa kuwa linahusisha na kuchanganya aina mbalimbali za sanaa kama muziki wa asili na kisasa, ngoma, maigizo, sarakasi, vichekesho, mazingaombwe, mashairi, maonyesho (exhibition) na sanaa zingine. Tamasha hili linatoa jukwaa la kipekee kwa wasanii wa ndani na kimataifa kushirikiana na kubadilishana uzoefu na ujuzi.

## SIFA ZA USHIRIKI:

TaSUBa inawakaribisha wasanii wa fani mbalimbali za sanaa na utamaduni kwa ajili ya kuomba kushiriki katika Tamasha. Iwe wewe ni mwimbaji, mwanamuziki, mchekeshaji, msanii wa sanaa za ufundi (mchoraji, mchonga sanamu), au mtaalamu mwingine wa ubunifu, tunakaribisha maombi yako ya kushiriki katika Tamasha.

## JINSI YA KUOMBA:

- Tembelea Tovuti yetu: Tembelea tovuti ya TaSUBa www.tasuba.ac.tz kupata habari za kina kuhusu Tamasha, ikiwa ni pamoja na mchakato wa maombi, na miongozo ya Tamasha.

- Jaza Fomu ya Maombi: Nenda kwenye sehemu ya "Tamasha" kwenye tovuti na upakue fomu ya maombi. Jaza kwa usahihi kuhusu taarifa Msanii/Kikundi na maelezo mengine.
- Mwisho wa Maombi: Mwisho wa kuwasilisha maombi ya kushiriki Tamasha ni **Agosti 31, 2026.**

**UTARATIBU WA MAOMBI YA USHIRIKI:**

Ili kupata nafasi ya ushiriki, tafadhali wasilisha yafuatayo:

- Fomu kamili ya Maombi:
- Maelezo ya Msanii: Maelezo mafupi kuhusu Msanii/Kikundi (Artist Biography).
- Wasilisha kazi yako: Ambatanisha picha au video fupi za kazi zako au viungo (links) kwenye portfolia au maonyesho ya mtandaoni yanayoonyesha mtindo wako wa sanaa.

**MCHAKATO WA MCHUJO:**

Kamati ya Tamasha itapitia kwa makini maombi yote na kuchagua wasanii/vikundi ambao kazi zao zitaonekana kuendana na malengo na mandhari ya Tamasha. Wasanii wote watakaopata na kukosa nafasi ya kufanya onyesho watapewa taarifa ifikapo **Septemba 30, 2026.**

**FAIDA KWA WASANII WATAKAOCHAGULIWA:**

i. Kukutana na kufanya onyesho katika hadhira kubwa yenye mchanganyiko tofauti.
ii. Fursa za kujenga mtandao na wasanii wengine na wadau wa sanaa na utamaduni.

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana

Barua pepe: bagamoyofest@tasuba.ac.tz au bagamoyofest@gmail.com

Tovuti: www.tasuba.ac.tz

Simu: +255(0) 755 853 436, +255(0) 714 510 386, na +255(0) 788 840 405

Dkt. Herbert F. Makoye

**MKUU WA CHUO - TaSUBa**